

THE HANSARD

Tuesday 12th August, 2025

Assembly Building

The Assembly met at 2.30 p.m

[The Speaker (Hon. Mohamed Roba) in the Chair]

PRAYERS

Hon. Speaker: Order Clerk.

MOTION

INSECURITY INCIDENTENCES IN THE COUNTY

(BY HON. PETER LOSU)

Hon. Peter Losu (Ngaremara): Thank you, Mr. Speaker. I beg to move a Motion; That aware that security is a function of the National Government according to the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya;

Further aware of the violent invasion of the County Assembly during the Impeachment proceedings, leading to vandalism of the Chamber, Assembly Offices and the Injuries of Staff;

Concerned that criminals are exploiting political turmoil and that insecurity incidences have grown beyond the Assembly events and extended to the communities;

Further concerned that insecurity underscores deep concern over violent threats aimed at local leaders, public officials and the general public, undermining the County governance processes;

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

Therefore, this House resolves that the relevant National Government agencies to;

- a) Put in place steps to guarantee the safety of the residents and the Members of the County Assembly, and
- b) Conduct an assessment of these insecurity cases to forestall such occurrences.

Thank you, Mr. Speaker.

Hon. Speaker: Secunder.

Hon. Meja Golicha (Chari): I stand to Second the Motion.

(Question Proposed)

Hon. Speaker: The floor is open for debate. Yes, Hon. Losu.

Hon. Peter Losu (Ngaremara): Asante Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kunipa hii nafasi, na pia nimeleta Hoja hii kwa sababu ya vurugu ambayo tumeshuhudia hapa. Mheshimiwa Spika, yale ambayo tunashuhudia katika Kaunti, ni kitu hatujawahi shuhudia hata wakati ule tulikuwa tunazozana hapo awali. Lakini wakati tulileta mjadala wa kuweza kung'atua Gavana mamlakani, Mheshimiwa Spika tumekuwa na shida na tunajua ya kwamba, hata kabla hayo, tumekuwa na shida ambayo iliyoweza kuchangia mmoja wetu, Mheshimiwa Nicholas Lorot, ambaye ni Mwakilishi Wadi wa Burat kuweza kupigwa risasi. Mheshimiwa Spika, kutoka huo wakati hadi saa hii, Isiolo haijakuwa katika ile hali ambayo imekuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, siku mbili iliyopita, mzee wetu tunayemheshimu sana, ambaye ni Karani katika baraza la wazee wa Kisomali, ndugu wetu Idle Hassan, ailiweza pia kupigwa risasi mbele ya Msikiti ya Jamia. Mheshimiwa Spika, hata jana jioni kulikuwa na kisa ambayo ilitendeka hapa kijiji cha LMD, na kuna mtu aliyeponea chupuchupu, yeye pia angekuwa kwa ile orodha ya wale waliopigwa risasi. Mheshimiwa Spika, tunaona kana kwamba kama Kaunti tunaelekea mahali pabaya, hatuendi kwa mpagilio ambayo inapaswa kuwa ya kiusalama. Mheshimiwa Spika, tunajua ya kwamba mambo ya kiusalama, sisi kama Serikali ya Kaunti ama ya Gatuzi, hatujapewa mamlaka kulingana na Sheria na Katiba ya Kenya ya kuweza kusimamia maadili ya Usalama. Lakini Mheshimiwa Spika tunajua ya kwamba kuna wale ambao wametunukiwa hilo jukumu katika Kaunti ambao ni Baraza la Usalama la Gatuzi.

Mheshimiwa Spika, tunajua hivi majuzi, wale waliokuwa wanahudumu kwa ile muda; pengine wamekaa sana katika Kaunti ya Isiolo waliweza kuondolewa. Hawakuondolewa ati kwa sababu walikuwa wanafanya kazi zao, ni kwa sababu walizembea na hata kuleta mgawanyiko katika Kaunti ya Isiolo, na pia kuleta kupendelea wananchi wengine kuliko wengine; na ndio maana waliweza kutolewa katika Kaunti ya Isiolo. Mheshimiwa Spika, ningepomba sisi kama Wana Bunge na pia kama Wana Isiolo tuchukue jukumu la Usalama kama yetu. Tusichukue kana kwamba kuna wale wamepewa hiyo majukumu peke yao tuwaachie. Ni vizuri sisi pia tuweze kujilinda. Kutoka wakati huo ambao tulileta mjadala wa kumng'atua Gavana mamlakani, tumekuwa na shida sana, na watu wameweza kulalama katika kila Wadi na pia katika Vitongoji mbali mbali katika mji wetu wa Isiolo. Kumekuwa na lalamishi mingi kwamba kumekuwa na hali ya kutokuwa na usalama katika Kaunti yetu. Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni kitu cha maana sisi pia kama Wana Bunge na Viongozi ambao wanawakilisha watu katika Kaunti ya Isiolo, wajitokeze ili sote tuweze kuhubiri amani; kwa sababu hatutaweza kuendelea na vile mambo ilivyo. Tukiwa tunajua kwamba sasa sio wakati wa siasa. Ikiwa pengine tutaingia katika machafuko ambayo tunaona sasa, na je ikifika wakati wa siasa tutaendelea namna gani?

Tunaona kana kwamba Mheshimiwa Spika, vile tunavyoendelea tunaweza kuwa na shida hata Zaidi. Kwa hivyo, ningepomba sisi sote tuweze kushirikiana pamoja na Viongozi wengine na wale wanaosimamia usalama katika Kaunti ya Isiolo, tushikane mkono tuweze kujadili na kuongea mambo ya usalama katika Kaunti yetu. Asante.

Hon. Speaker: Mheshimiwa Kiambi.

Hon. Salesio Kiambi (Wabera): Asante Mheshimiwa Spika, kwa kunipea nafasi hii niweze kuchangia hii ajenda ya usalama katika Kaunti yetu. Hata kabla ya *Impeachment*, hatukuwa na usalama, kwa sababu kuna mwenzetu alipigwa risasi, ambaye ni Mheshimiwa Nicholas Lorot. Na pia wakati tulifanya mambo ya *Impeachment*, tukaenda mahali kutayarisha mambo ya kusikiza hayo maneno katika Seneti, kuna mwenzetu aliyelitwa Abdirahman, alichukuliwa na majambazi wengine Kaunti zingine, na inaweza kuwa watu wa hii Kaunti, walitufuata.

Kwa hivyo usalama ya hapa Isiolo ni mbaya. Mheshimiwa Spika, hivi majuzi hapa Bula Pesa, Kambi ya Juu, kuna mama alipigwa risasi na Ng'ombe wake pia wakapigwa risasi. Hawa watu walipiga hiyo boma risasi, hawakuiba chochote, walikuwa na nia ingine. Kwa hivyo, hapa Isiolo ukosefu wa usalama

ni mbaya. Hata kama wale wako hapa walinzi kutoka Serikali Kuu, tunafaa tuongezewe na wale walikuja wageni, wapange mikakati ya usalama hapa mji wa Isiolo, na pia mashinani, kwa sababu tuko na uoga. Juzi nilikuwa natembea hapa Kiwanjani nikisalimia watu, wakaniambia hata kuna sehemu ingine wezi wanakaa, tuje tukae mkutano ili wanielezee ni wapi na huyu mtu ni nani, wnakaa na kundi ya wakora ambao kazi yao ni kuiba usiku. Hapa Isiolo ni kubaya, hata sisi wenyewe na raia wote tuna uoga. Na hii inafaa ichukuliwe kipa umbele na mikakati ipangwe vizuri. Mheshimiwa Spika ningomba hata sisi kama Wakilishi Wadi na pia wewe, tutembelee *Commissioner* na tumueleze ile shida iko Isiolo. Kwa sababu huyu *Commissioner* wa Kaunti ni mgeni na labda hajajua vile Isiolo iko. Tuweze kumuelezea sehemu fulani iko namna hii, ili aweze kupanga mikakati ya usalama. *Officers* wawe wakipiga *patrol* katika hii Isiolo town na Mashinani pia kila Wadi, ili wananchi waweze kupata usalama ya kutosha. Mheshimiwa Spika, naunga hii Hoja mkono. Asante sana.

Hon. Speaker: Honourable Lorot.

Hon. Nicholas Lorot (Burat): Asante Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia katika hii Hoja ya ukosefu wa usalama. Kifungo cha Mia Mbili Thelathini na Nane cha Katiba ya Kenya, inazungumzia kwamba ni wajibu ya Serikali tukufu iliyo mamlakani kuweza kulinda na kuweka usalama kwa wananchi wa Kenya wakifanya biashara, maandamano na kazi zao, ni wajibu wao. Mheshimiwa Spika, Isiolo usalama umeharibika katika hali kubwa sana. Hapo awali Isiolo tulikuwa tunajua mambo ya uvamizi ya Ng'ombe, Mbuji, Ngamia, ndio ilikuwa inaendelea katika Kaunti ya Isiolo. Sasa hiyo uvamizi umetoka hapo, na kuingia sasa kuwinda wale Viongozi.

Mheshimiwa Spika kama vile mimi tarehe Ishirini na Sita Mwezi wa Tatu niliweza kupigwa katika hoteli ya Galaxy na kulikuwa na tabia ya watu wa pikipiki kuandama wale Viongozi. Ilikuwa wale wanalengwa walikuwa wale wanazungumzia haswa mambo ya Kaunti ya Isiolo, na hiyo ni njia moja ya kuuzia watu wa Isiolo uoga kuweza kufunga wale ambao wanatetea haki ya wananchi kutoongea. Mheshimiwa Spika, uchunguzi huo wangu, kulikuwa na ile *footage*, sijui kwa Kiswahili tutaita aje. Huo uchunguzi haujaenda hadi wa leo. Tumeweza kuisukuma lakini haijasonga, imeweza kusimama pale pale mahali tuliacha. Mheshimiwa Spika, ugefuatiliwa na ule mhalifu aweze kupatikana ingekuwa ni vyema, tungeweza kujua ni nani ambaye ako nyuma ya haya maneno ya kupiga watu risasi.

Mheshimiwa Spika, unaona juzi wakati nilipigwa risasi, haijapita muda mrefu, mzee amepigwa, ambaye ni Karani wa Wasomali. Na hivi kwangu, kuna mama aliyepoteza maisha; na hapo jana tena LMD. Kwa hivyo ni kitu kinachoendelea

sasa. Hali yetu kama Waheshimiwa, ambao tunasimama na wananchi wetu wa Isiolo na kutetea haki yao ya kimandeleo, maisha yetu iko hatarini. Na sisi hatuna wale walinzi, kama wale Wabunge wa Serikali Kuu wanapewa. Kwa hivyo sisi tumeambiwa tujulinde na hata hatuna silaha. Kama sisi wengine tume *apply* zile silaha ndogo ndogo na imechukua muda ya kuweza kupata. Kwa hivyo, siku hizi town kwetu imekuwa mahame, ikifika saa kumi, watu wanaanza kutoroka town, na hapa usalama unafaa uwe wa masaa Ishirini na nne. Ni mahali watu wanafanya biashara na shughuli muhimu, infaa usalama hapa. Kwa hivyo, tungeomba Polisi, NIS, na wale ambao ni wauhusika wa usalama waweze kuweka doria kali katika mji wetu wa Isiolo, kuweza kujua ni nini inaendelea katika Kaunti.

Mheshimiwa Spika, uliona vile Assembl yetu iliweza kubomolewa, ilivunjwa mchana peupe, na kuna hata camera inaonyesha wale waliovunja. Zile magari zilikuwa hapa pia zilivunjwa, zikaporwa. Sergeant at arm wetu aliweza kupigwa na akanyang'anywa mace, Hansard iliharibiwa na pia pia mtu wa wetu wa picha alipigwa na kuchukuliwa camera. Na wale waliofanya hiyo kitendo wanajulikana. Mheshimiwa Spika, mpaka leo hawa watu hawajachukuliwa hatua na Sheria. Kwa hivyo, tunasema usalama wa Isiolo umedorora na ni mbaya. Tungeomba wale Viongozi wahusika na *Security* wa Kenya kama Inspector General (IG), waweze kuingilia mambo ya Isiolo na kuchunguza ni nini inaendelea Kaunti ya Isiolo.

Mheshimiwa Spika, nilishangaa juzi kwa matamshi ingine Kiongozi ailiweza kutoa, kwa yule mzee aliyepigwa risasi. Niliona katika mtandao Kiongozi akisema ni OLF. Tungependa huyo Kiongozi aweze kueleza kinagaubaga ya kwamba hawa OLF wako wapi? Nani aliyepiga huyo mzee? Kwa sababu kuongea mitandaoni na itabaki hapo, hiyo ni kuchochea. Infaa Kiongozi aje katika kituo cha Polisi, apige ripoti yake, aeleze hawa OLF wako wapi. Sisi wengine tungependa kujua hawa OLF wako wapi? Kama ni OLF wanafanya hizi vitu inafaa washikwe; kwa sababu sisi wengine hivi leo tunabeba risasi, tumekuwa walemavu na tunalaani hicho kitendo. Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika hili sio jambo la mzaha, ni jambo ambalo tunaomba Serikali Kuu ambayo iko na jukumu ya ulinzi wa wananchi, iweze kuamka kuhakikisha Isiolo usalama umerejea katika hali ya kawaida. Kwa sababu haya mambo haijawahi tendeka Isiolo, hatujawahi ona, watu ama Viongozi wakipigwa mchana risasi. Na hapo awali tulikuwa tukiongea silaha kidogo kidogo imeingia hapa, ilmeletwa na wale wahalifu walikuwa wanauza ile dawa za kulevya. Waziri wa usalama kuna wakati alisema Isiolo atahakikisha wale wahalifu wameshikwa, na mpaka leo hatujaona watu wameshikwa. Tungeomba Waziri wa Ndani ya Ulinzi wa Kitaifa, Murkomen aweze kuvalia viatu mambo ya Isiolo.

Mheshimiwa Spika, naunga hii Hoja mkono, na ni mjadala mzuri ambayo inafaa itiliwe maanani. Sisi wakati tulileta hiyo mambo ya *Impeachment*, tangu hiyo siku mpaka wa leo, usalama hapa haijakuwa mzuri. Sisi wale wengine tulikimbizwa, tuliona Abdirahman, ule ambaye alikuwa *Chief Officer* wa Afya, hajapata haki yake mpaka wa leo. Tungeomba Abdirahman apate haki yake, wale waliohusika wawe wameshikwa, wamepelekwa korokoni na wameshtakiwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, sisi tunataka mambo ya usalama itiliwe mkazo. Asante sana.

Hon. Speaker: Honourable Dekha

Hon. Dekha Bonja (Nominated): Asante Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Mimi pia nimesimama kuunga huu mjadala mkono. Mheshimiwa Spika, usalama ni kitu muhimu. Kama hatuna usalama hatuwezi kukaa vizuri. Mimi kama mama, usalama ni muhimu kwangu na pia kwa watoto wangu na jamii. Kwa sababu usalama unapokosekana, ule mtu ako na shida sana ni mama, kwa vile tuna watoto nyumbani; shida inapotokea, hatujui vile tutakimbia na hawa watoto kutafuta usalama wetu. Mheshimiwa Spika, risasi inapigwa kila wakati, na hujui ni kwa nini zinapigwa. Sasa Mheshimiwa Spika, mahali ambapo ina usalama ni pale mtu anaenda kuomba Mwenyezi Mungu, kama Msikitini ndio mtu anapigwa risasi, ni wapi ndio tuna usalama? Hapa Isiolo yetu ambayo ilikuwa mzuri, ni wapi tuko na usalama?

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, tunahofia maisha yetu na ya watu wetu wa Isiolo. Jamii inatuangalia kama Viongozi, na ni vizuri sisi mpaka wale wako Serikali Kuu na wa Kaunti tujaribu kukashifu haya maneno yanayoendelea katika Isiolo yetu, tuhakikishe tuko na Amani. Na wale ambao wako hapa kwa mambo ya usalama, waje kutulinda, kwa sababu ni haki yetu sisi kuwa na Amani katika Nchi yetu; sisi hatuko Nchi ingine Mheshimiwa Spika, tuko hapa Kenya, na inapaswa pia sisi tuangaliwe vile wengine wana usalama, pia sisi tuwe nayo. Serikali yetu ya juu waweze kutuangalia. Mpaka CS wetu Murkomen, aangalie usalama wetu Mheshimiwa Spika. Hiyo ndio sisi tunaongea kwa hii Nyumba, tunasema, tunahitaji usalama kama watu wa Isiolo, kwa sababu sisi pia ni Wakenya na tunahitaji pia tuwe na amani na tufanye kazi yetu kwa njia ya amani.

Hapa Assembly, hatuna ile usalama, uliona Mheshimiwa Spika wakati ule tulikuwa tunajadili mambo ya *Impeachment*, tumeingiliwa hapa na vijana wakitupiga na mawe; hayo maneno yetu mpaka saa hizi haijaangaliwa, hakuna kitu mbaya ambayo sisi tumefanya, ni kazi yetu ambayo Katiba imetupa ruhusu tuifanye. Sisi hatuna ofisi, ama mahali pa kukaa Mheshimiwa Spika. Yaani hiyo shida yote ni kwa sababu ya kukosa usalama ndio imetuletea. Na ni Viongozi

wengine ndio wanatuletea hizi shida. Kwa hivyo, ni vizuri Viongozi wetu wa Isiolo na pia wa juu tushikane tujaribu kutafuta usalama Mheshimiwa Spika. Na usalama inatoka kama Viongozi kwanza. Kama Viongozi watakuwa wanongea kiholela, watafanya jamii yetu wapigane na wataleta shida baina yao. Sisi watu wa Isiolo ni jamii moja, ambao sisi sote tunapendana, makabila zote ziko hapa, sisi ni kama watoto wa mama moja tukiwa hapa Isiolo; na sisi tunapendana. Hatutaki Viongozi wengine waje watugawanye kwa sababu ya siasa yao. Kwa kutafuta chakula, watu wasitupiganishe sisi watu wetu wa Isiolo. Asante Mheshimiwa Spika.

Hon. Speaker: Honourable Kamila.

Hon. Kamila Warsame (Nominated): Thank you, Mr. Speaker. I stand to support the Motion on insecurity incidents in the County. Mr. Speaker, it is good for all of us to understand the genesis of the insecurity of Isiolo. When was it started? Where are we today, Mr. Speaker? Mr. Speaker, we were initially prone to issues of cattle rustling and any other thing which occurs outside the Municipality. But the insecurity of today, Mr. Speaker, we are talking about, has come now to the issues which occurs within the Municipality, Mr. Speaker. Mr. Speaker, these incidents begun when we started the issue of Impeachment of the Governor. I remember very well, Mr. Speaker, on 18th of June, when the Members of County Assembly came here to table the second Impeachment Motion, that is when this insecurity started. We were actually removed from this premises of Assembly by hammered vehicle, Mr. Speaker. And it was in public domain that the security of Members of County Assembly was at risk. Mr. Speaker, the same day, the vandalization of these premises, the structures in these premises also occurred the same day, Mr. Speaker. In the eyes of the security personnel, Mr. Speaker, they were just here, nothing has been done. They went into each and every office in this County Assembly, Mr. Speaker, distracted by former Clerk, Salad Boru, plus the Governor of Isiolo County. Mr. Speaker, before then, Abdirahman Afey, who was former Chief Officer for the Health, Mr. Speaker, was beaten to the level we cannot understand, Mr. Speaker. He was hospitalized, Mr. Speaker. Nothing has been done.

Mr. Speaker. The other incident, the killing of Mr. Abdikadir Happy, Mr. Speaker, took place in Isiolo. He was burnt beyond recognition, Mr. Speaker, buried and nothing was done on his investigation, Mr. Speaker. The blogger, called Ismail Abdikadir. If I am not wrong, Mr. Speaker was also injured. He was literally beaten, forming the crack, which was on his head, was what each and every person in this, not only in Isiolo, but this Nation at large, discovered that that person was beaten. But the issue is changed, that the guy was, the

accident was caused by a vehicle, which you cannot tell even a small baby, Mr. Speaker. You can just read from the injuries that occurred that person, he was not injured by a vehicle, Mr. Speaker, and nothing has been done. My colleague, Honorable Nicholas Lorot, Mr. Speaker, he was shot by several bullets, Mr. Speaker, nothing has been done as well, and the investigation was done. It has taken process, but we are not seeing any outcome, Mr. Speaker. We really wonder, are we belonging to the Country of Kenya? Why is it that justice is not given to the people of Isiolo? That is the question we are asking the CS, Internal Security, Mr. Murkomen, to give justice to the people of Isiolo.

Mr. Speaker, recently, the Secretary General, Mr. Idle Hassan, who is Secretary General to the community of Somali, I can say former, because he was taken from that position, he was injured also. This incident occurred Weeks, after fortnight, after a Month, but nothing has taking place. Now, when I'm standing and speaking, Mr. Speaker, even I'm feeling for myself. I may be even shot to death because of what I'm discussing in this House. Our security is at risk, Mr. Speaker, we are even fearing to talk about issues of Isiolo as Elected and Nominated Members of this County Assembly, because we are really feeling for ourselves and for our people at large. Our Senator is always in the Senate House discussing the security of Isiolo, Mr. Speaker. Why is it that the issue of Isiolo is not taken seriously? We really want to go to this President and even the Ministers who are concerned with this, Mr. Speaker, to ask what is really going on as far as the issue of Isiolo is concerned. Because the issue of people buying with money, we don't have money to buy people, Mr. Speaker. We voted this Government. We have been voted by our people to speak on their behalf. We have our National Representative, Mr. Speaker. Like our Senator, she's always talking on our behalf, but her voice, we appreciate at some level, Mr. Speaker. Let me not say we don't appreciate the Government, but at some point we appreciate. But the issue which is reaching, the process of investigation is starting, reaching some level, yet we are not seeing.

People are talking, why is their insecurity? Insecurity happens because of injustices which are occurring in this place. The former Clerk made some fake forgeries and the name of our Speaker was removed. That is what has resulted to some of the insecurities, Mr. Speaker. People are talking about issues of insecurity. If people are not practicing their rights, Mr. Speaker, how do we expect that people just listen and stay like that. We are feeling pain, Mr. Speaker. I'm really pained when the former Clerk and even the Governor their issues of bringing those people into books, it has not taken place, Mr. Speaker. It is just justice denied for us, Mr. Speaker. And I support this Motion and I want this Motion to be implemented as far as this resolution is concerned. And we are very sorry for ourselves and I appreciate the Motion Mover. Thank you.

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

Hon. Speaker: Honourable Abubakar.

Hon. Abubakar Godana (Sericho): Mr. Speaker, as a Nation, the key mandate of a State is to make sure that every life is protected. And I feel as a Nation, this regime has failed all of us. Because matters of security cannot be compromised, it's not negotiable. In Isiolo, the recent happenings in the insecurity issues are attributed to the top leadership of Isiolo County, more so Governorship. The era, the goonship and the trend of the happenings. Hon. Lorot was beaten by someone on a motorcycle, came and hit him, ran away. Mr. Idle, likewise; if you see the trend, this is a borrowed habit from the City in Nairobi, which was never in Isiolo before. The history of Isiolo was about Cattle rustling and the communities checking on each other, like when Cattle from Borana are taken by Turkana, we retaliate, it was just a friendly matter. But this time around, it's matters of security, where hit men come with a motorbike and hit you and run away. You can never trace them. The Government agencies have slept with the leadership. No justice has been served to Hon. Lorot MCA of Burat up to now, Mr. Idle, likewise. Mr. Abdikadir Happi, all these lives were lost. So when you see all this, it's either Government siding with the leadership, or there's something wrong with the entire system of Kenya.

During the past regimes, matters of security were very sensitive and the matters of Constitution were taken seriously, Government makes sure that they don't play around with matters of Constitution and Constitutionalism. Issues of forgery with our former Clerk, Salad Boru, he forged our signatures. In his statement, he said that the Election of the fake Speaker happened during the 26th, which was the day we Impeached the Governor. In his Affidavit, which is in the Senate, and I must be quoted very clearly, in his Affidavit, which is in the senate, he swore an Affidavit saying that there was no Sitting which took place on the 26th. Then how comes the same Clerk alleges that there was Election of a fake Speaker on the same 26th? Actually, all these matters are a security failure. We have reported all these issues to the relevant authorities, and no action has been taken from there. So the Clerk is still roaming around saying he's still the Clerk. In reality, he's a criminal who needs to be in jail. Then I'm appealing to the Minister, Murkomen, that our lives, even the nine Members who are with the Speaker, are at risk, and we can be shot anytime from now. I must be put on record that nine of us, our lives are at risk, and anytime from now, anytime from now, one of us will be a victim next. So as a Government, when leaders, we are not any other person, we are leaders, we represent the entire region, entire certain area of our County; and when we raise these issues, it must be taken seriously. Every now and then, we complain that no action is being taken. Is the Government of Kenya functioning? When our entire

leadership raises such issues, and says that our lives are at risk, and no one is taking up those issues.

We have real issues like Hon. Lorot, who has been complaining for the last Five Months, he has been complaining that he knows there's a lead to his case. He has a lead. He has a message to that effect, saying that he has crossed the red line. Is there an action taken? No. Abdirahman, we were there, actually all of us who are witnesses, 16 of us, at the Maanzoni, 16 State Officers were witnesses, plus the Speaker 17; 17 State Officers were witnessing the action. These are not ordinary persons, these are State Officers who are Gazetted, and their words cannot be taken lightly. So as a matter of urgency, we are raising these issues for ourselves and for the general public. No one should die while the Government is watching. Death is a natural thing, it is God -given, but death by the hands of any other person, a crooked person, it should not be accepted, Mr. Speaker. We should not accept that. And we should even go International, not National; If the Government will not listen to us, will not listen to our cries, we are crying every now and then to the radios, to the public, to every corner, that our lives are at risk. And the next morning you'll see that someone else is a victim.

So as a matter of urgency, we are urging the entire humanity, not even Kenya, the International people who are of concern to these matters, that as Isiolo, we Members plus our Speaker, our life is at high risk. Actually, the Country is turning into a Banana Republic. What's the difference between Kenya and Somalia when the Government cannot even protect their Gazetted Officers? These are people who are Constitutionally mandated, given powers to carry out some duties. So Mr. Speaker, I support the Motion, and it's a timely one, before anyone else leaves us, so that you leave while your head is held high, because you have raised your issues. Thank you, Mr. Speaker.

Hon. Speaker: Mover you can reply.

Hon. Peter Losu (Ngaremara): Nashukuru sana Mstahiki Spika kwa sababu ya kunipa nafasi nyingine na nachukua pia fursa hii kuwashukuru Wabunge wenzangu kwa sababu ya kuweza kujadili na pia kuibua Hoja ambayo tumekuwa nayo katika Kaunti yetu ya Isiolo. Mheshimiwa Spika, yale yaliyosemwa na Wabunge ni maneno ambayo ni ya haki na ya kweli, mambo ambayo imekuwa ikiendelea katika Kaunti ya Isiolo. Mheshimiwa Spika, katika Katiba yetu, ni jukumu la Serikali Kuu kuweza kuchunga watu na mali yao. Kwa hivyo, vile tunavyoendelea kulingana na misururu na mashumbulio na pia hali ya kupoteza maisha katika Kaunti ya Isiolo imekuwa ni jambo imeleta utatata na pia tumbo joto katika wakaazi wa Isiolo. Ningeomba Mheshimiwa

Spika, sisi sote tuweze kushirikiana. Kwa sababu hali ya usalama katika Isiolo, haswa katika town imekuwa hali ambayo ni tatanishi sana. Mheshimiwa Spika, tukiendelea namna hii, hiyo inamaanisha ya kwamba hatutakuwa na usalama na watu wetu pengine mwishowe watakuja kuvurugana ama hata kukoseana heshima kwa njia moja.

Mheshimiwa Spika, tungeomba vitengo vya Serikali ambayo inahusika na mambo ya usalama, waweze kuchukua hatua na pia kufanya uchunguzi wa kina ili kuweza kuibua na kujua ni yapi yanaendelea katika Kaunti ya Isiolo. Pia Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao hawajapata haki kuanzia Mheshimiwa Lorot, yule mama aliyeweza kuuwawa na Ng'ombe wake hapo Kambi ya Juu, ndugu wetu Happi, ndugu yetu aliyejeruhiwa na mwisho akafa na pia mzee wetu Idle, na wale wengine mpaka hata ile kisa ya jana; tungeomba wafanyikazi wa Serikali ambao wanasimamia hali ya usalama katika Kaunti ya Isiolo, waweze kufanya uchunguzi wa kina ili tuweze kujua ni nini inaendelea katika Kaunti ya Isiolo. Mheshimiwa Spika, bila kusahau ya kwamba hii Kaunti ya Isiolo iko na silaha mingi ambazo ni haramu. Mheshimiwa Spika, ikiwa silaha iko kwa mikono ambayo haijaweza kupewa idhini ama cheti cha kumiliki hicho silaha na kuweza kutumiwa kwa njia ambayo inapaswa, kuna uwezekano wa machafuko kuwa katika Kaunti ya Isiolo. Kwa hivyo tungeomba hata Serikali pia iweze kuharakisha, kwa wale pia wangehitaji cheti ya kumiliki silaha katika Kenya ama Kaunti, kwa vile tunajua sisi kama Wabunge wa Kaunti, mimi pia nikiwa mmoja wao, tuliweza kupeana hilo ombi ya kupewa cheti ya kuweza kumiliki silaha katika Kenya. Lakini Mheshimiwa Spika, hiyo kitu imechukua muda, nafikiri kwa sasa imechukua Miezi Tano imepita. Mheshimiwa Spika, tunaona kidogo pia sio jambo nzuri. Ikiwa sisi pia wale tunaitwa Wabunge wa Kaunti tunapigwa risasi, je wananchi watakuwa wapi? Hiyo inaleta hali ya taharuki katika vitongoji tunavyoishi. Kwa sababu Mheshimiwa Spika, pengine wakati mambo ya mashambulizi inafikia Viongozi, ni vitu ambayo haijawahi fanyika katika Kaunti ya Isiolo. Na pia yale ambayo yanaendelea saa hii kulenga, ya kuweza kupiga Viongozi ama wazee ambao tunaotegemea katika jamii kwa kutoa maoni ama hata kuelekeza jamii. Mheshimiwa Spika, ile kiwango tuliofika ni ambayo haijawahi kuwa katika Isiolo, na tunaona ya kwamba hii ni tabia ambayo inafanyika katika town kubwa. Lakini ukiona vile imefika Isiolo, tunaona ya kwamba hatukuwa tumejipanga kama wana Isiolo; hiyo ni tabia ambayo imeweza kuja juzi Mheshimiwa Spika. Na tungeomba Serikali Kuu pamoja na Viongozi wote tuweze kufaulu kwa yale ambayo yanaendelea, na pia wafanye uchunguzi, na wale ambao wanahusika, waweze kufikishwa kwa Sheria. Kwa sababu tusipofanya hivyo, Serikali haitakuwa inafanya kazi yake. Lazima wachukue wajibu ya kuweza kuchunga watu na mali yao.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kiwango ya uharibifu uliofanyika katika Bunge yetu, hiyo ni kitu kinachofanyika kwa Nchi ambayo haina Serikali. Ikiwa Kenya itaendelea vile jinsi ambavyo vitu vinatekelezwa, ina maanisha ya kwamba pengine Mwananchi wa kawaida hatakuwa na budi ila kujichunga. Mheshimiwa Spika, ikifika wakati Mwananchi wa kawaida anachukua hatua ama jukumu ya kuweza kujilinda, ina maanisha ya kuwa hakuna Serikali ambayo ina uwezo wa kumlinda. Kwa hivyo, tungeomba Serikali Kuu pamoja na Serikali ya Kaunti waweze kuchukua jukumu ya kuwalinda Wananchi wa Isiolo pamoja na mali yao. Nashukuru sana, asanti.

Hon. Speaker: Honorable Members, I now put the question; that aware that security is a function of the National Government according to the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya;

Further aware of the violent invasion of the Assembly during the Impeachment proceedings leading to vandalism of the Chamber, Assembly Offices and the Injuries of Staff;

Concerned that criminals are exploiting political turmoil and that insecurity incidences have grown beyond the Assembly events and extended to the communities;

Further, concerned that the insecurity underscores deep concern over violent threats aimed at local leaders, public officials and the general public, undermining the County governance processes;

Therefore, this House resolves that the relevant National Government agencies to;

- a) Put in place steps to guarantee the safety of the residents and the Members of the County Assembly, and
- b) Conduct an assessment of these insecurity cases to forestall such occurrences.

(Question Put and Agreed to)

Next Order!

MOTION

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

SHORT -TERM BORROWING FOR CASH MANAGEMENT TO PAY
SALARIES
(HON. ABUBAKAR GODANA)

Hon. Abubakar Godana (Sericho): Thank you, Mr. Speaker, Motion on short term borrowing for cash management to pay salaries,

That Aware that, Section 142 of the Public Finance Management Act, 2012 provides that the County Assembly may authorize short-term borrowing by County Government entities for cash management purposes only;

Further aware that such borrowing approved by the County Assembly is repaid within the same Financial Year;

Concerned that delays in disbursement of funds have resulted in cash flow challenges in the County Government, thereby affecting timely payment of Salaries and other Statutory obligations;

Noting that delayed payment of salaries to the County employees has negative impact on service delivery, staff morale and overall economic activity in the County.

Now, therefore, this Assembly resolves;

- a) To authorize the County Assembly Service Board to undertake short-term borrowing within the limits prescribed by the Public Finance Management Act, 2012, for the purpose of cash management to meet salary obligations.
- b) That the borrowing shall be repaid within the same Financial Year in accordance with Section 142 (3) of the Act.

Hon. Speaker: Secunder?

Hon. Nicholas Lorot (Burat): I stand to Second the Motion.

(Question Proposed)

Hon. Speaker: The floor is open for debate.

Hon. Abubakar Godana (Sericho): Thank you Hon. Speaker. I rise on behalf of the dedicated County Assembly Fraternity. Article 207 of the Constitution

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

and Section 109 of the Public Finance Management Act (PFMA) establish the County Revenue Fund, from which all County expenditures are made. However, Honorable Members, despite our Budgetary approvals, the actual flow of funds is sometimes disrupted by delays in the disbursement of Equitable Share from the National Treasury. This has created cash flow challenges in our County, most notably affecting the timely payment of salaries. Honorable Members, when salaries are delayed, their impact is immediate:

1. Public servants are unable to meet their obligations;
2. Morale drops down;
3. Service delivery suffers.; and
4. The local economy slows down.

The Public Finance Management Act, 2012, under Section 142 (1) recognizes that such situations can occur and therefore, allows County entities to borrow short-term for cash flow management. Section 140 (2) makes it clear that this borrowing must be approved by the County Assembly and Section 142 (3) of the same requires that the borrowing is repaid within the same Financial Year.

Honorable Speaker, I beg that;

- (i) The House approve short-term borrowing by the County Assembly Service Board strictly within the limits set under Section 142 (3),
- (ii) Ensure that the borrowing is for the sole purpose of paying salaries.

This is not a proposal for long -term debt. Honorable Members, it is a temporary measure to safeguard our Assembly's service delivery and to protect the welfare of our employees.

Let us remember that a demoralized workforce cannot deliver on our County's development agenda. Approving this Motion is not only lawful under the PFMA and the County Governments Act, but it is also a responsible action in the interest of Good Governance and Fiscal Management.

I therefore urge all the Members to support this Motion.

Hon. Speaker: Honourable Losu.

Hon. Peter Losu (Ngaremara): Thank you Mr. Speaker. I think the Motion is very clear. I don't think I have a lot to discuss on the same. In a way Mr. Speaker, we as the Board have been given the same mandate by the Act. Whenever we face a crisis like we are now, Mr. Speaker, we have no option

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

other than to look on the Act to where maybe we have been permitted by the Act. Mr. Speaker, we will be working within the confines of the Law. And so, Mr. Speaker, I think as the Board, we are ready to do that and to also make our Members comfortable and the entire staff. I thank you.

Hon. Speaker: Honourable Lorot.

Hon. Nicholas Lorot (Burat): Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa hii nafasi kuweza kuchangia ukopaji wa County Assembly ili kuweza kuwalipa wafanyikazi ukiwa mishahara inachelewa. Mheshimiwa Spika, wafanyikazi wa Assembly wamevunjika moyo sana kwa sababu ya mishahara yao kuchelewa kwa Miezi mbili, tatu, kwa sababu ya Serikali Kuu kuachilia ile mgao katika Kaunti. Kama vile unvyojua, wafanyikazi wa Assembly na Waheshimiwa ni wazazi, wako na wanafunzi wanasoma katika shule za upili, Chuo kikuu na Mheshimiwa Spika, kwa kuchelewa kwa mishahara, wengi wanahangaika. Unakuta wanafunzi wanarejeshwa nyumbani, wengi wanachukua mkopo, wanauza mifugo kuweza kulipa karo, na ilhali wewe ni mfanyikazi. Hiyo inafanya watu kuvunjika moyo wa kufanya kazi. Na ni vyema kuweza kuwatia wafanyikazi wa Assembly moyo kwa mishahara wao kuingia kwa wakati unaofaa.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, tunaomba ukopaji kwa ile asilimia ndogo ya kukopa. Hivyo basi tunaunga mkono ili wafanyikazi na Waheshimiwa waweze kupata mishahara yao kwa wakati unaofaa ili waweze kutekeleza majukumu yao ya nyumbani vilivyo. Kwa sababu mtu anapofanya kazi, anafaa kupata haki yake kwa wakati unaofaa; wako na familia na jukumu nyingi. Mheshimiwa Spika, nilipata habari hivi Juzi kwamba kuna mfanyikazi wetu mmoja ailiweza kupoteza familia yake kwa sababu ya kukosa pesa ya kumpeleka hospitali. Kwa hiyo, kwa kuchelewa kwa mishahara, huyu mtu ailiweza kupoteza familia. Hiyo ni hali ya uchungu na ambayo hatutaweza kufurahia. Kwa sasa hivi, ile kadi yetu ya *Insurance*, kwa muda mrefu haifanyi kazi kwa vile haijalipiwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, unapokosa pesa ya kuenda hospitali mtu akigonjeka, hiyo hali ya maisha ni mbaya. Tungeomba Waheshimiwa waunge mkono kwa ukopaji ndogo ili iweze kusaidia wafanyikazi wetu na Waheshimiwa kuweza kufanya kazi yao kwa hali nzuri. Asanti sana Mheshimiwa Spika.

Hon. Speaker: Honourable Kiambi.

Hon. Salesio Kiambi (Wabera): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi nichangie hii Hoja muhimu kwa wafanyikazi na Waheshimiwa wetu. Unajua kila mtu ako na jukumu ambayo inawakumba watu wengi. Kwa hivyo,

DISCLAIMER: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

Mheshimiwa Spika, naunga mkono *Board* iweze kuomba pesa ili wafanyikazi waweze kupata mishahara. Na kuna hata wafanyakazi wengine hata huwa hawakuji Assembly, sijui hawa wanaweza kufanywa nini. Kwa sababu hapa tuko na wafanyikazi Mia Mbili, lakini hapo *Board* itaangalia tuone itakuwa namna gani. Kwa sababu kuna wengine ambao wako mrengo hii, na kuna wale walienda upande ule mwingine wa *former Clerk*, hapo ndio *Board* wataangalia itakuwa namna gani; wale wanaweza kulipwa na wale waliojifuta kazi wenyewe. Unajua kama mtu amejifuta kazi haifai alipwe. Pia ni muhimu *Board* ya Assembly iweze kuomba pesa hata nje ya Kaunti, hata kwa Serikali Kuu, kama vile tuliambiwa siku moja, tupate pesa ya kufanya *repair* kwa hii Assembly katika ofisi, kwa vile saa hii clerks wanabeba makaratasi kwa mfuko, hawawezi kuacha kwa ofisi kwa vile kwa saa hii sio kuzuri, inaweza hata ibiwa.

Hivyo basi ni mzuri hata hiyo pesa ya kurekebisha ofisi iweze kuombwa kwa vile naona wanapitia kazi ngumu, ambayo hata kuweka hizi *Order Paper* ni ngumu. Kwa hivyo, *Board* waharakishe na kuomba pesa ili tuweze kurekebisha haya mambo yote. Asanti Mheshimiwa Spika.

Hon. Speaker: Honorable Members, I now put the question; That Aware that, Section 142 of the Public Finance Management Act, 2012 provides that the County Assembly may authorize short-term borrowing by County Government entities for cash management purposes only;

Further aware that such borrowing approved by the County Assembly is repaid within the same Financial Year;

Concerned that delay in disbursement of funds have resulted in cash flow challenges in the County Government, thereby affecting timely payment of Salaries and other Statutory obligations;

Noting that delayed payment of salaries to the County employees has a negative impact on service delivery, staff morale and overall economic activity in the County.

Now, therefore, this Assembly resolves;

- a) To authorize the County Assembly Service Board to undertake short-term borrowing within the limits prescribed by the Public Finance Management Act, 2012 for the purpose of cash management to meet salary obligations.

- b) That the borrowing shall be repaid within the same Financial Year in accordance with Section 142 (3) of the Act.

(Question Put and Agreed to)

ADJOURNMENT

Hon. Speaker: Honorable Members, the House now remains adjourned until tomorrow Wednesday 13th August, 2025 at 9.00 a.m.

The House rose at 4.35 p.m.